Mkulima Mbunifu

Jarida la Kilimo Endelevu Afrika Mashariki

TOLEO MAALUMU, 5


Picha:MkM


Picha:MkM


Picha:MkM


Picha:MkM


Picha:MkM

# Wakulima vinara wa MkM ni mabalozi wa kilimo endelevu

*Nchini Tanzania, kilimo si kazi tu, ni sehemu ya maisha ya kila siku. Kilimo kinatoa ajira kwa takribani asilimia 80 ya Watanzania na kuchangia takribani asilimia 30 ya pato la taifa. Kiasi kikubwa cha chakula chetu kinazalishwa na wakulima wadogo. Hata hivyo, licha ya mchango wao mkubwa, wakulima hawa hukumbwa na changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na udongo kupoteza rutuba, hali ya hewa isiyotabirika, bei zisizo na uhakika sokoni, na ukosefu wa taarifa sahihi na kwa wakati kuhusu kilimo.*

Hii ni moja ya sababu kubwa ya Mkulima Mbunifu (MkM), kutafuta suluhisho kwa maswala yanayowakumba wakulima wadogo, kuwapa maarifa ya kilimo ili kupanua uzalishaji na kuinua hali ya maisha.

Mradi wa MkM unatoa maarifa ya kilimo yanayofanya kazi, na hili limethibitishwa na wakulima wanufaika wa mradi huu. Wakulima hawa wanatoa ushuhuda wa kuongezeka kwa mavuno na mapato, kukidhi mahitaji ya chakula safi na salama kwa familia, na kuboreshwa kwa mazingira kupitia mbinu sahihi na endelevu shambani.

Toleo hili limetayarishwa na kuchapishwa na Mkulima Mbunifu
Mhariri: Erica Rugabandana, Mhariri Msaidizi: Flora Laanyuni,
Mpangilio: Cathbert Msemo
Mkulima Mbunifu: S. L. P. 14402, Arusha, Sakina, Barabara ya Majengo, Jengo la Elerai.
www.mkulimambunifu.org, barua pepe: info@mkulimambunifu.org
Rununu +255717 266007, +255766841366




Flora Laanyuni

# Kupitia jarida la MkM, nimeweza kufanya kilimo hai kibiashara

***Wakulima wengi wamenufaika kutokana na elimu ya bure inayotolewa kupitia jarida hili. Wanasoma na kufanyia majaribio mbinu mbalimbali zinazosimuliwa, uzoefu wa wakulima na watalamu wa kilimo endelevu.***



"Tangu mwaka wa 2012, nimekuwa msomaji wa jarida la Mkulima Mbunifu (MkM) na nimepiga hatua kubwa katika uzalishaji", hivyo ndivyo alivyoanza kujitanabaisha Bw. Godfrey Kimaro kutoka Karansi, mkoani Kilimanjaro, alipotembelewa na mwandishi wa jarida hili kwa lengo la kufahamu ni kwa namna gani jarida la Mkulima Mbunifu limekuwa nyenzo katika uzalishaji wa mazao na wanyama kwa wakulima na wanufaika katika eneo hilo.

> ***"Jarida la Mkulima Mbunifu limenisaidia kufahamu na kufanya kilimo ikolojia kwa ukubwa na kupata faida, hasa pale ninapozalisha kwa gharama nafuu, kupata mavuno mengi na kufikia soko kwa urahisi.***

Bw. Godfrey ambaye alionyesha furaha alipotembelewa, alitoa nakala mbalimbali za jarida ambazo amekuwa akipokea kuanzia mwaka 2012. Anasema kwamba amekuwa akizisoma na kuhifadhi, pia akitumia elimu hiyo kwa vitendo katika shughuli zake za uzalishaji. Anaendelea kusema kwamba MkM ni kama darasa kwa wakulima na linajibu changamoto nyingi za wakulima, kwa mfano, kuanzia kuweka malengo ya uzalishaji mpaka kufika kujenga na kudumisha soko.

"Nilianza rasmi kilimo biashara mwaka 2015 huku nikizalisha maharagwe, mahindi, ndizi na mbogamboga. Ingawa kwa uchache, ninafuga ng'ombe, kuku na mbuzi ambao kwa hakika wamekuwa msaada mkubwa kwangu kifedha na kwa chakula kwa familia yangu", anasimulia.

## Kabla ya jarida

"Mimi nilikuwa nafanya kilimo, japo kwa kiasi kidogo, lakini nilikuwa nafanya kilimo cha asili yaani natumia mbegu za asili, mbolea za wanyama, hivyo sikuwahi kutumia kabisa mbinu za kisasa kama madawa, mbegu na mbolea katika kuzalisha", anaeleza.

Anasema kwamba jarida la Mkulima Mbunifu limemsaidia kufahamu na kufanya kilimo ikolojia kwa ukubwa na kupata faida, hasa pale anapozalisha kwa gharama nafuu, kupata mavuno mengi na kufikia soko kwa urahisi.

"Kupitia jarida hili, nimejifunza kufanya kilimo cha matuta ambacho toka awali sikuwa nakifahamu kabisa. Nimejifunza kufanya kilimo cha mbogamboga kwa ukubwa na kwa njia ya kibiashara. Nimeweza kufahamu aina za

malisho, namna ya kuzalisha, kulisha mifugo na namna ya kutengeneza na kutumia aina mbalimbali za dawa za asili ", Godfrey anaeleza.

"Aidha, nimeweza kujifunza kuhusu ufugaji wa kuku wa asili na kuanza mradi huo. Nimejifunza namna ya kuwapa chanjo kutoka vifaranga wanapoanguliwa mpaka wanapokuwa kuku wakubwa, namna ya kuandaa na kulisha chakula cha kuku, kuweka na kutunza kumbukumbu za uzalishaji", anaendelea kusimulia.

Bw. Kimaro anasema kuwa yeye pamoja na wanakijiji wengine waliweza kutibu mifugo yao kutokana na ugonjwa wa mapele ngozi mara baada ya kusoma makala kwenye jarida la Septemba 2015, na mpaka sasa wanachanja mifugo yao kila mwaka na huo ugonjwa haupo tena.

Nimeweza kununua pikipiki ambayo naitumia katika shughuli zangu za kilimo na kupeleka mazao kwa wanunuzi, nimeweza kuchimba maji na kununua mipira ya matone ambayo natumia kufanya kilimo cha umwagiliaji kwa njia ya matone hasa katika msimu ambapo nakosa maji au kiangazi.

### Kuhusu wakulima wengine

Wakulima wengi wanaonizunguka ni wanufaika wa jarida na mara wanapopokea kwenye kikundi chao, wanasoma pamoja na kubadilishana mawazo, kwani jarida linagusa moja kwa moja shughuli wanazofanya na linatatua changamoto zao hapo kwa hapo.

### Changamoto katika kilimo

"Kila penye faida, changamoto hazikosekani na changamoto kubwa ninayokumbana nayo ni ukame, hivyo imenilazimu kuchimba maji ardhini ambayo natumia katika uzalishaji na hunigharimu kuweka umeme kwa ajili ya kupandisha maji na kusambaza shambani", anasema. Aidha anapanda mazao yanayostahimili ukame ili kuendeleza uzalishaji kwa mwaka mzima.

### Wito kwa MkM

Bw. Godfrey anasema, "Naomba sana wadau wa jarida hili kututembelea mara kwa mara, kwanza kujionea kazi tunazozifanya, lakini pia kushauriana mambo kadhaa yanayotusumbua shambani kwani kuna maswali mengine tunaona tungeweza kupatiwa majibu sahihi ikiwa mtu amejionea mwenyewe kwa macho kile tungependa kuuliza."

### Wito kwa wakulima

"Ningependa kuwashauri wakulima wenzangu kupenda kujisomea jarida hili mara wanapolipata, pia kuhifadhi nakala hizi kwa matumizi ya baadaye kwani mimi mpaka sasa nina nakala zangu zote tokea mwaka 2012 na mara kwa mara, narejelea kusoma pale ninapohitaji msaada.



Erica Rugabandana

# Kilimo ikolojia imenijengea heshima na marafiki

***"Jina langu ni Rehema Mbura, kutoka kijiji cha Ilongero, kata ya Ilongero. Mimi ni mkulima wa kiikolojia na ninalima mtama, mahindi, alizeti na mboga mboga. Pia mimi ni mfugaji, ninafuga ng'ombe, kuku na mbuzi.***

***Nilianza kupokea jarida la Mkulima Mbunifu mwaka wa 2021. Ninapokea na kusambaza ndani na nje ya kata ya Ilongero.***

Nimejikita katika matumizi ya mbinu za kiikolojia, kwa sababu ninapata chakula kingi, salama na ardhi yangu inakuwa katika ubora. Kilimo hiki kimeniwekea mazingira mazuri na afya zetu zinakuwa salama.

## Ufugaji wa kuku

Ninafuga kuku aina ya sasso ambao ninawatoa Arusha au Iringa. Nikishawapokea wale kuku, mimi ninawalisha kiikolojia na wananipatia nyama tamu sana. Idadi ya kuku ninaowafuga zaidi ya 200 au 300 kulingana na uwezo wangu. Mbuzi na ng'ombe ni wachache, ila ninawafuga pia kiikolojia. Haya yote ninafanya kwa shamba ekari 6.5.

## Teknolojia

Nimejifunza vitu vingi kupitia jarida la MkM. Kwanza, ni jinsi ya kutengeneza viuatilifu, kitu ambacho kimenisaidia sana. Nilikuwa nategemea kununua viuatilifu kutoka madukani lakini majarida yamenipa mwongozo mzuri kwani mimi na wanakikundi tunatengeneza viuatilifu vyetu wenyewe. Viuatilifu hivi havigharimu, kwani tunatengeneza kwa kutumia malighafi yanayopatikana katika maeneo yetu na tunahakikisha tunazalisha dawa ambayo haiangamizi wadudu rafiki.

Pia, tumejifunza kuhusu ufugaji na tunaweza kutengeneza madawa ya asili kwa ajili ya mifugo yetu. Kwa mfano, dawa ya kuwasaidia kuku kupambana na magonjwa. Jarida limetujenga sana na watu wanafanya vitu vingi sana kupitia jarida la Mkulima Mbunifu.

## Mafanikio

Nimepata mafanikio mengi lakini la kwanza ni elimu; Elimu hii imetujengea uwezo sisi wakulima kubadilisha hali tuliyokuwa nayo na kurudi kwa uhalisia wa kilimo.

Pili, tumerutubisha ardhi; Ardhi ilikuwa imechoka, imelimwa tangu kitambo mpaka sisi wakulima wa sasa tumeikuta. Sasa hivi, tunajitahidi kurutubisha na kudumisha rutuba ya udongo na tunawasaidia wakulima wengine ili kunusuru changamoto ya mmomonyoko wa ardhi na gharama ambazo hazifai.

Tunapanda mbogamboga kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na ziada tunauza; Kwa wale wakulima ambao hawana ardhi ya kutosha tunawafundisha kutumia vyombo kama ndoo, gunia na vifaa vingine vinavyohitaji eneo ndogo ili kupanda mbogamboga. Pia, tunapanda miti kwa wingi na hii hupelekea kuwa na mandhari nzuri na hewa safi vijijini.



Picha:MkM

Kwa upande wangu, nimejenga kipato na kupanua ufugaji wa kuku, ng'ombe, shamba, na imenijengea heshima kwa wengine. HAidha ninawatembelea wakulima, na shule kutoa mafunzo kwa walimu na wanafunzi kuhusu kilimo ikolojia.

## Kuwashirikisha wakulima

Natoa elimu kupitia vikundi mbalimbali wanaonialika, na pia kupitia mikutano ya hadhara, wakinipa nafasi natoa ushauri. Natumia fursa hizi kusambaza taarifa na jarida la MkM. Ninapoenda kwenye maeneo ya wakulima, nawasiliana na viongozi na wananipa nafasi ya kutoa mafunzo. Ila, vikundi vya wakulima wanaweza kunialika moja kwa moja na nakubali mualiko na kwenda kuwafundisha na hadi sasa nimewafikia watu zaidi ya 450.

Kitu ambacho kimewavutia wakulima ni kilimo cha mbogamboga kwa sababu kinachangia usalama wa chakula cha nyumbani na ni chanzo haraka cha kipato, kwani huchukua muda mfupi kukua na kurudisha faida kwa mzalishaji.

## Ushauri na matarajio

"Itakuwa vizuri kwa wadau na serikali wakifanya kazi kwa pamoja kujenga benki ya mbegu za asili ili kuwawezesha wakulima kufikia na kuzalisha mbegu hizi na kupunguza gharama ya pembejeo."alisema.



Picha:MkM

> ***Nimepata mafanikio mengi lakini la kwanza ni elimu; Elimu hii imetujengea uwezo sisi wakulima kubadilisha hali tuliyokuwa nayo na kurudi kwa uhalisia wa kilimo.***

Magreth Mollel

# Mbinu bora za kilimo-ikolojia kwa wakulima wadogo

***Kilimo ikolojia kinatoa njia kwa wakulima wadogo kufikia mifumo imara ya kilimo endelevu. Mbinu hizi zinaweka kipaumbele usawa wa kiikolojia, uanuwai, na matumizi madogo ya pembejeo za nje, na kusababisha mazingira yenye afya, maisha bora, na uhakika wa chakula. Ingawa kuna mbinu nyingi zenye manufaa, tunaangazia mbinu muhimu kwa wakulima wadogo zinazosambazwa na kutumiwa na wakulima wanaopokea makala za MkM.***

## Kupanda mazao kwa maseto

Badala ya kulima zao moja tu, wakulima wanapanda mazao mengi katika eneo moja au kwa mzunguko na huongeza uanuwai wa kibiolojia juu na chini ya udongo. Kwa kuchanganya mazao mawili au zaidi wakulima wanapata faida. Kwa mfano, jamii ya kunde (kama maharagwe) inapopandwa pamoja na nafaka (kama mahindi) inaongeza naitrojeni kwenye udongo, na kunufaisha zao la nafaka.

Mazao tofauti pia huvutia aina mbalimbali za wadudu. Hii imeonekana kuvuruga mzunguko wa wadudu waharibifu na kumpatia mkulima mavuno zaidi, hupunguza hatari ya kupoteza mazao yote kutokana na mashambulizi ya wadudu au magonjwa. Kupitia mbinu hii wakulima wenye eneo dogo wameweza kuboresha matumizi ya rasilimali na kuongeza uzalishaji kwa kila eneo.



Picha:MkM

## Usimamizi jumuishi wa wadudu na magonjwa

Mbinu hii inalenga kuzuia milipuko ya wadudu na magonjwa badala ya kutegemea dawa za wadudu. Hii inahusisha mchanganyiko wa mikakati kama vile kuchagua aina ya mazao/mbegu zinazostahimili magonjwa, mzunguko wa mazao ili kuvunja mzunguko wa wadudu, kutumia wadudu marafiki, kutumia vyombo vinavyowavutia na kuwanasa wadudu waharibifu, na ikibidi mkulima atawaondoa wadudu waharibifu akitumia mikono.

Watumiaji wa mazao ya kilimo wameonekana kushabikia na kununua bidhaa kutoka kwa wakulima wanaozalisha kwa njia hii. Pia, ni gharama nafuu kwa mzalishaji na inapunguza hatari za kimazingira na kiafya zinazohusiana na matumizi ya dawa za wadudu za kemikali.

## Mbinu zinazohifadhi maji

Uhaba wa maji ni changamoto kwa wakulima wadogo walio wengi. Wakulima wanakusanya ama kuvuna maji msimu wa mvua kwa kujenga mabwawa madogo kwa ajili ya umwagiliaji wakati wa kiangazi, wanatengeneza matuta ya kontua, matandazo ya majani makavu au mabaki ya mimea ili kuhifadhi unyevu kwenye udongo, na kutumia njia bora za umwagiliaji kama vile umwagiliaji wa matone. Pia, wanachagua aina ya mazao zinazostahimili ukame.



Picha:MkM

## Kipindi cha mpito

Ingawa faida za kilimo-ikolojia ni kubwa, kipindi cha mpito, yaani kubadilisha kutoka kilimo cha kawaida, kinaweza kuleta changamoto kwa wakulima wadogo.

- Katika hatua za mwanzo, mavuno yanaweza kupungua kwa muda mfupi wakati harakati asili za kurutubisha udongo zinapotekelezwa, kupunguza kutegemea pembejeo za kemikali, na kuweka mikakati mwafaka ya usimamizi.
- Baadhi ya mbinu za kilimo-ikolojia, kama vile kutengeneza samadi na kupalilia kwa mikono, zinaweza kuhitaji nguvu kazi nyingi zaidi kuliko mbinu za kawaida.
- Wakulima wanaweza kukosa maarifa na ujuzi unaohitajika kutekeleza mbinu hizi kwa ufanisi, na huduma za ugani zinaweza kuwa hazitoshi kutoa msaada unaohitajika kwa wakati unaofaa.
- Kupata masoko ya bidhaa za kilimo hai na kukidhi mahitaji ya uthibitishaji kunaweza kuwa changamoto na gharama kwa wakulima wadogo. Pia, ukosefu wa sera zinazounga mkono na kupiga jeki wakulima wadogo inaweza kuzuia kilimo ikolojia kuenea na kuwafikia wakulima wengi.



Picha:MkM

Flora Laanyuni

# Jarida la Mkulima Mbunifu limeniwezesha kufanya kilimo ikolojia na kuzalisha kwa tija

***Kama ilivyo ada, Mkulima Mbunifu tumeendelea kuwatembelea wakulima na wanufaika wa jarida hili kufahamu ni kwa namna gani elimu wanayoipata kupitia makala za kila mwezi zimeendelea kuleta chachu katika shughuli zao za kilimo na hata kuweza kuwabadilisha kimaisha.***

Bw. Adili Msangi kutoka Karatu (Arusha) ni miongoni mwa wanufaika wa jarida la MkM na anaeleza kuwa amejifunza mengi kupitia makala mbalimbali kuzalisha kwa misingi ya kilimo ikolojia katika ufugaji wa kuku, nguruwe, pamoja na kilimo cha mahindi, maharage, matunda, mbogamboga na uzalishaji wa miche ya matunda.

Bw. Adili anaeleza kuwa, ameweza kufanya shughuli zake za kilimo na ufugaji kwa ufanisi mkubwa, na kwa njia za kitaalamu zaidi kwa muda mfupi toka kuanza kusoma jarida la MkM ambapo alianza kupokea nakala ya kwanza mwaka 2017 mpaka sasa. Aidha, elimu itolewayo kwenye jarida hili imemuwezesha kubadilisha mtindo wa uzalishaji toka katika kilimo mamboleo hadi kilimo ikolojia katika eneo lake dogo la nusu ya robo ya ekari.

## Kwanini kilimo ikolojia na jarida la MkM

"Mimi nilianza kufanya kilimo mwaka 2016 lakini nilikuwa nafanya kilimo mamboleo natumia pembejeo za viwandani zenye kemikali lakini mara baada ya kupokea jarida la MkM kupitia MVIWAA (Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Arusha) nilianza kufanya kilimo na ufugaji kwa njia ya ikolojia jambo ambalo najivunia kutokana na faida nilizopata hadi sasa kupitia elimu itolewayo na jarida hili".

Nilikuwa nikikumbana na changamoto mbalimbali katika kilimo hasa gharama za manunuzi ya pembejeo za kilimo kama vile mbegu, mbolea na dawa ambazo kila wakati wa msimu wa kilimo hulazimika kuingia mfukoni na kwenda dukani kununua.

Nimejifunza njia rahisi ya uzalishaji wa mboga salama iliyozalishwa na kukuzwa kwa njia ya asili bila kutumia kemikali.




## Faida zingine alizopata kupitia jarida

- Nimepata fursa ya kuunganishwa na kukutana na wakulima wengine kutoka mikoa mbalimbali.
- Nimeweza kuwa mkufunzi wa kufundisha wakulima wengine kilimo ikolojia ambapo nimeweza kuwafikia wakulima 100 na wanafanya ufugaji wa kuku, nguruwe, kilimo cha mbogamboga, mahindi, maharage, matunda.
- Nimeweza kuanza mkakati wa kuwafundisha wanafunzi na natarajia kufikia wanafunzi 30 katika shule moja.




- Nimeweza kuzalisha chakula safi na salama chenye lishe kamili.
- Nimefanikiwa kuzalisha na kusambaza mbegu kwa wakulima mbalimbali ndani na nje ya Karatu.
- Nimeweza kuchaguliwa kuwa namba moja na kupewa Tsh. Milioni 5 miongoni mwa wakulima wa Wilaya ya Karatu na Ngorongoro katika uandishi wa mpango kazi wa ufugaji wa kuku.
- Nimefanikiwa kupata fedha na kuweza kusomesha watoto, kujenga makazi bora, kuchimba kisima cha maji cha lita 40,000 pamoja na kujilipia ada ya shule na kusomea cheti cha kilimo na ufugaji wa samaki.

## Vipi kuhusu soko la mazao ya ikolojia

Bw. Adili anaeleza kuwa, soko la mazao yake ni wananchi waliyomzunguka lakini pia anauza kwa wakulima kutoka sehemu mbalimbali ndani ya wilaya ya Karatu na hata mikoani kwani wengi hununua hasa mbegu za mahindi na maharage lakini pia nguruwe na kuku.

Anaongeza kuwa, anajivunia kuwa mzalishaji wa kilimo ikolojia kwani hata faida anayoipata kwasasa ni kubwa ukilingania na mwanzoni alipokuwa akifanya kilimo mamboleo. Katika eneo lake la nusu ya robo ya ekari alikuwa akifanya mauzo kwa mwaka anapata si chini ya Tsh. Milioni 1.5 lakini kwasasa katika eneo lilelile anapata mpaka Tsh. Milioni 4.5.

## Changamoto


"Changamoto kubwa ninayoipata ni kukosa usafiri wa kudumu na wa haraka ambao ungeniwezesha hasa kuwatembelea na kuwafundisha wakulima wengi lakini pia kusafirisha bidhaa au mazao kwenda kwa wanunuzi". alisema


## Ushauri kwa Mkulima Mbunifu

Bw. Adili anasema kuwa, anashauri Mkulima Mbunifu kuhakikisha wanapeleka elimu hii ya kilimo ikolojia kwa wakulima wengi bila kujua ni yupi atafanya au hatofanya lakini kikubwa wapate elimu na watambue madhara yatokanayo na kilimo cha kisasa chenye kutumia kemikali za viwandani zenye sumu.




*Mkulima Mbunifu ilipotembelea kikundi cha wakulima Rangaha sale kufanya mahojiano kuhusiana na mada za gazeti la Mkulima Mbunifu pia kuwasikiliza wakulima changamoto wanazokutana nazo katika kutekeleza shughuli za kilimo, ili kupata ufumbuzi.*



Erica Rugabandana




# Wakulima ni mabalozi wa kilimo endelevu

***Wakulima wanaofaidika na MkM wameweza kunufaika kwa kutumia mbinu wanazojifunza na kutumia kuboresha uzalishaji wao. Baadhi yao wamepata jukumu la kuwafundisha na kuwaonesha maarifa wakulima wenzao katika maeneo yao.***

Huu ni ushirikiano mkubwa wa kuharakisha utumiaji wa mbinu endelevu. Wakulima hawa vinara ni wakulima wadogo waliofanikiwa kutumia mbinu za kilimo hai na kujenga biashara endelevu za kilimo. Hawa ni mifano bora katika jamii zao. MkM huwapatia mafunzo ya ziada na kuwasaidia kufungua mashamba yao kama vituo vya kujifunzia maeneo ambapo wakulima wengine wanaweza kuona na kujifunza kwa vitendo.

Mfumo huu umejibu moja kwa moja kilio cha wasomaji wa jarida la MkM wanaotaka zaidi ya maandishi yaani wanataka kuona, kugusa, na kujaribu wenyewe.

Kwa sasa, MkM inashirikiana na zaidi ya wakulima vinara 63 kutoka mikoa lengwa na kwingineko. Mbali na kufundisha, wakulima vinara huchangia pia maudhui ya jarida, husambaza nakala, na kuwezesha masomo na kujifunza kutoka mkulima kwa mkulima.

Wakulima vinara wa MkM wana majukumu mbalimbali muhimu.

### Kuonesha mbinu bora za kilimo hai

Wanatunza mashamba yao vizuri na mashamba haya ni mifano yanayoonesha mbinu bora kama kutengeneza mboji, mchanganyiko wa mazao, kulima miti na mazao kwa mchanganyiko (*agroforestry*), na udhibiti wa wadudu kwa njia asilia.

### Kutoa mafunzo na ushauri kwa wakulima wenzao

Wanatoa mafunzo ya vitendo na maonesho mashambani, hasa kuhusu utengenezaji na matumizi ya viuatilifu asilia na pembejeo nafuu zinazopatikana kirahisi. Ili kuchochea mafunzo ya wakulima kwa wakulima, wanaratibu mikutano ya wakulima katika jamii, na ziara za kubadilishana uzoefu.

### Kusambaza taarifa ya MkM

Wanawafikishia wakulima magazeti ya Mkulima Mbunifu na moduli mbalimbali za mafunzo hata kwa wakulima walioko maeneo ya mbali. Pia, wanakusanya maoni kuhusu taarifa za MkM na vile jarida linaweza kuboreshwa zaidi. Wanatuma picha, mafanikio, changamoto, na suluhisho ili kusaidia kuandaa makala kwa matoleo yajayo ya jarida.

### Kuimarisha ushirikiano na maafisa ugani

Wanashirikiana na maafisa ugani wa serikali, wauzaji wa pembejeo na wadau wengine kuimarisha ushauri wa kilimo.




> ***MkM huwapatia mafunzo ya ziada na kuwasaidia kufungua mashamba yao kama vituo vya kujifunzia. Haya ni maeneo ambapo wakulima wengine wanaweza kuona na kujifunza kwa vitendo.***

## Mfumo endelevu wa mabadiliko

Mfumo huu wa wakulima vinara wa MkM umebuniwa kwa lengo la kuleta mafanikio si sasa tu bali pia kudumisha mabadiliko ya baadaye. Hawa ni mawakala wa mabadiliko walioko mashinani, wanaobuni na kusambaza maarifa na suluhisho kwa changamoto zinazowakabili wakulima wadogo.

Kazi yao inaziba pengo kati ya maarifa na vitendo, kati ya kurasa za jarida na mashamba halisi.

Kadri Tanzania inavyoendelea kukumbatia kilimo hai, Wakulima vinara wa MkM wanathibitisha kuwa mabadiliko ya kweli yanawezekana na yanaanzia kijijini.




*Mkulima Mbunifu kwa Wanafunzi*

Erica Rugabandana

# Dawa ni ya kuwafukuza wadudu, sio kuwaua

***"Mimi ni Manase Meoki, mkulima kutoka kijiji cha olchorovus kata ya Musa, Wilaya ya Arusha DC, (Arusha). Ninalima nikitumia mbinu za ki-ikolojia na nimejifunza kupitia kikundi cha wakulima kinachojulikana kama Esupat. Katika kikundi chetu tumejifunza mbinu mbalimbali kama vile kuweka matandazo kwenye udongo na kuweka makinga-maji ili kuzuia mmomonyoko wa udongo.***

Katika shamba langu ninalima mazao ya migomba (mashina 85), mihogo na viazi lishe vya asili, parachichi 160, paipai 12, miwa na mahindi ya asili, maharagwe, kunde na mbogamboga (spinach, sukuma wiki, mnafu) na kitunguu. Ninafanya haya yote kwa shamba la ekari 4. Ninazalisha bila kutumia mbolea ya chumvichumvi au kemikali sumu, ninatengeneza dawa za asili sio ya kuwaua wadudu bali ya kuwafukuza wadudu waharibifu huku nikidumisha wale wadudu wazuri.

## Mafunzo

Nilianza kupokea jarida la MkM mwaka wa 2023. Nimejifunza mambo kadhaa;

- Kwanza, namna ya kutunza afya ya udongo, mfano, zamani nilikuwa nachoma majani wakati ninasafisha na kutayarisha shamba, lakini nimejifunza kuyatunza ili kurejesha rutuba kwenye shamba.
- Pili, ni namna ya kuchanganya mazao ili nikianguka kwenye zao moja, zao lingine litafanya vizuri.
- Tatu, kuna mazao ambayo yanategemeana, kwa mfano, ukiweka maharagwe kwenye mahindi, maharagwe yanarutubisha udongo, kwa hivyo, unakuta mahindi yananawiri. Kwa pande mwingine, mahindi yanazuia upepo na kulinda maharagwe.
- Nne, jambo la uhifadhi na usalama wa chakula, kwamba tunahitaji tukitunze kile tunachovuna kwa matumizi ya baadaye. Njia moja asili ya kutunza nafaka ni kutumia majivu ya mgomba yasivamiwe na wadudu wakati wa kuhifadhi.

## Mafanikio

Nimepata mafanikio mengi, mfano;

- Zamani, tulikuwa tunakumba na uhaba wa chakula kwa sababu uzalishaji ulikuwa mdogo. Baada ya kutunza afya ya udongo, tunapata chakula cha kutosha na ya kuuza ili kufanya maendeleo mengine ya kupanua uzalishaji. Nimeweza kupanda parachichi kutokana na mauzo ya mazao mengine.
- Kutokana na mauzo ya ndizi nimeweza kununua mtambo wa solar na runinga dishi/mtambo wa kupokea matangazo ama picha kwenye runinga. Hivi ni vitu ambavyo nisingeweza kununua bila kupata hela shambani.
- Watu wanaonizunguka wameona mabadiliko katika hali yangu ya maisha. Majirani ununua chakula wakati ambapo kuna upungufu wa chakula, majirani ununua chakula kutoka shamba langu. Wengi wao wanataka kujifunza kwangu, kwamba kama mimi ninaweza kununua, pia nao wanaweza kununua.



## Wakulima wengine

Nimefungua shamba darasa kwangu nyumbani la kufunza mbinu mbalimbali za kilimo ikolojia, na ninatoa mafunzo kwa wakulima binafsi, vikundi vya wakulima, makanisa, na wanafunzi wa shule za msingi na ya upili. Pia, napokea vikundi kutoka nje ya kata.

Nimetenga sehemu ya mafunzo; kuna vitu ambayo havina faida kwangu lakini navitunza kwa ajili ya mafunzo kwa wengine.

Nimeweza kuwafikia zaidi ya wakulima 1,000. Kitu ambacho kimefanya watu waniamini ni kwamba mwaka jana, nilikuwa mshindi wa pili kwenye maonyesho ya Nane-Nane kwenye Halmashauri ya Arusha DC. Hivyo, watu wana taka sana kujua ni kwa nini mimi ni mkulima bora.

## Kinachovutia

Kitu ambacho kimenivutia sana kwenye jarida ni kwamba kila taarifa ina picha. Kwa hivyo, lile niliona kwa picha nitafanya kwa usahihi kuliko kusoma tu kwenye maandishi. Wakati mwingine, nikitaka kufanya jambo, ninaangalia picha na kufanya jambo kama ilivyo kwenye picha.

## Mipango

Ningependa kuwateua wakulima kumi ambao nitawafunza halafu na wao wanaendeleza kile ambacho wamejifunza. Tunakuwa kama timu ambayo mimi ninasimamia ili tuweze kuwafikia wakulima wengi zaidi. Pia, ningependa kutengeneza vipindi vya redio na televisheni/runinga kuhusu mbinu mbalimbali za kilimo ikolojia. Ninalenga kuwafikia wakulima 10,000.

## Wito

Ninahimiza serikali kuweka mifumo rafiki kwa wakulima wadogo ambao ni wazalishaji wa chakula chetu ili wakulima waweze kuzijua. Pia, wakulima watumie pembejeo za asili na watengenezewe pahali pa kuzipata pembejeo hizi kwa bei nafuu."



Picha:MkM

*Ningependa kuwateua wakulima kumi ambao nitawafunza halafu na wao wanaendeleza kile ambacho wamejifunza. Tunakuwa kama timu ambayo mimi ninasimamia ili tuweze kuwafikia wakulima wengi zaidi.*



Flora Laanyuni

# Kupanda miti ili kuhifadhi mazingira

***Kukatwa kwa miti au misitu inasababisha ukame na ongezeko la joto. Ili kukabiliana na hali hii, wakulima wanapanda miti ili kukidhi mahitaji ya kawi (kuni), mbao ya ujenzi na matumizi mengine. Hii hufanyika na kufanikiwa zaidi wakati wa mvua.***

MkM imekuwa mstari wa mbele kuwahamasisha wakulima na wananchi kwa ujumla juu ya umuhimu wa kuhifadhi mazingira. Wakulima wanachangia ukataji wa miti kwa ajili ya kuongeza ukubwa wa mashamba ya mazao hasa ya chakula, na hii inaleta dalili za mabadiliko ya tabianchi. Tunavyosema, ukikata mti moja, hakikisha unapanda miti mengine miwili.

Miti huwa na faida nyingi, hasa miti ya matunda ambayo huimarisha lishe ya familia kwa sababu ni chanzo cha vitamin na virutubisho muhimu kwa mwili, pia miti ya lishe kwa mifugo, miti ya kuzuia mmomonyoko wa udongo, na kuwa chanzo cha mapato kwa mkulima anapouza kwa ajili ya mbao kuni, na mambo mengine.

Kuna manufaa mengine yasiyoleta hela lakini huchangia mandhari kuwa nzuri, kwa mfano, kupungua hewa ya ukaa na kuleta hewa safi, kupunguza ongezeko la joto, na kuboresha mkusanyiko wa mawingu ya mvua, kuimarisha utunzaji wa maji aridhini katika maeneo ya mashambani.

Kwa kawaida, wakulima wanaona ni heri kupanda miti ya matunda kwa sababu miti ya matunda itakuwa na thamani kubwa kwa familia. Hivyo si rahisi kukatwa kwa matumizi mengine (kama vile kuni au makaa). Elimu ya uzalishaji wa miche na utunzaji mzuri wa bustani za miti za matunda imewawezesha wakulima kuweza kutunza miti na kupata manufaa yayoambatana na kuwa na bustani ya miti shambani.


Picha:IN

biovision

mkulimambunifu.org,
theorganicfarmer.org
infonet-biovision.org

+255 717 266 007
http://www.facebook.com/mkulima_mbunifu
http://twitter.com/mkulima_mbunifu
https://www.instagramu.com/mkulima_mbunifu

Biovision Africa Trust

Haki zote zimehifadhiwa ©2023 *Mkulima Mbunifu*